

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Mkoa wa Dodoma  
Anwani ya Simu REGCOM  
Simu: 026 2324343/2324384  
Nukushi:0262320046/2320121  
Barua pepe : [ras@dodoma.go.tz](mailto:ras@dodoma.go.tz)



*Ofisi ya Mkuu wa Mkoa*  
**S.L.P. 914**  
**Dodoma**

---

**TAARIFA YA AWALI YA SERIKALI YA MKOA WA DODOMA KWA VYOMBO VYA HABARI  
JUU YA TUKIO LA MBUNGE WA SINGIDA MASHARIKI MHE. TUNDU LISSU  
KUSHAMBULIWA KWA RISASI**

Kufuatia tukio la Mbunge wa Singida Mashariki (CHADEMA) Mheshimiwa Tundu Lissu kushambuliwa na risasi na watu wasiojulikana eneo la "Area D" Mjini Dodoma leo Septemba 7, 2017 majira ya mchana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Jordan Rugimbana amewataka wananchi wa Dodoma kuwa na subira, utulivu na kuendelea na shughuli zao wakati huu ambao tayari Jeshi la Polisi limeanza kazi ya uchunguzi na msako juu ya tukio lililotokea na wahusika walioshiriki kutenda tukio hilo na kuahidi kuwa taarifa zitaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Rugimbana amewataka wananchi kufahamu kuwa kwa sasa Mheshimiwa Lissu anaendelea kupatiwa matibabu ya haraka kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma na uongozi wa hospitali umeelekeza wananchi na viongozi mbalimbali watoe nafasi kwa Wataalamu wa Afya kumhudumia Mheshimiwa Lissu.

*"Nitoe wito kwa wakazi wa Mkoa wa Dodoma tuendeleo kusubiri taarifa kutoka Jeshi la Polisi wakati huu ambao wanachukua hatua mbalimbali, lakini pia niwaombe sana wananchi wenye nia njema wanaotaka kuja kumwona Mheshimiwa Lissu na kumjulia hali kwenye hospitali ya Mkoa wa Dodoma wasifanye hivyo kwa sasa kwa kuwa eneo la hospitali ni finyu na tusingependelea mikusanyiko na hata katika maeneo ya Mji wa Dodoma kwa kuwa bado Jeshi la Polisi linafuatilia kujua asili ya tukio lenyewe na mikusanyiko ya watu mara nyingine inaweza kutumika vibaya hata kwa wale wanaofuatiliwa ili kujua chanzo na sababu za tukio lililotokea "***Amesema Mkuu wa Mkoa Rugimbana.**

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma Afande Gilles Muroto ameomba mwananchi yoyote mwenye taarifa yoyote kuhusu tukio lililotokea atoe taarifa kwa Jeshi la Polisi na kuwa tayari wameanza uchunguzi wa tukio, wameshaweka vizuizi nje ya mji kwa lengo la kuendelea kuchunguza kilichotokea. Aidha, ameongeza kuwa taarifa za awali zinaonesha kuwa gari iliyohusika ni aina ya Nissan nyeupe lakini hawajaweza kufahamu namba zake za usajili hivyo wanaendelea kufuatilia.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. James Charles amewajulisha waandishi wa habari kuwa hali ya Mheshimiwa Lissu iko imara na timu ya Madaktari Bingwa wanaendelea kumpatia huduma ya matibabu na kuwa wanao uwezo wa kutosha wa kutoa huduma ya dharura ya Afya.

  
Jeremiah Mwakyo

**AFISA HABARI NA UHUSIANO - OFISI YA MKUU WA MKOA DODOMA**

**Septemba 7, 2017**